

# MUDA WA HADITHI ZA MAANDIKO

**Na Norman Hill**  
(Imetokana na hadithi ya kweli)

*Hadithi hii iliokea huko Ghana.*

**H**uu ni wakati wa kusoma," Bw. Otoo alisema. Nyameye aliketi wima. Muda wa kusoma ni burudani!

Kila siku shulen, mwalimu wao alisoma kitabu kwa sauti darasani. Wakati mwininge alisoma kuhusu wanyama. Wakati mwininge alisoma kuhusu watu katika nchi zingine. Na wakati mwininge aliuliza darasa kama walikuwa na kitabu wangetaka yeye asome.

"Je, kuna mtu yeyote aliye na kitabu anataka nikisome leo?" Bw. Otoo aliuliza.

Nyameye alinyanya mkono wake.

"Ninacho!" Alitwaa mkoba wake na kutoa kitabu chake anachokipenda. Ilikuwa ni kitabu cha hadithi za Kitabu cha Mormoni! Alikileta ili kukisoma baada ya shule wakati akimsubiri mama yake kumchukua. Kuona picha hizi kulimsaidia kuelewa hadithi za maandiko.

*"Je, kuna mtu yeyote  
aliye na kitabu  
anataka nikisome leo?"  
Bw. Otoo aliuliza.*

Bw. Otoo alitabasamu wakati alipoona kitabu kikubwa. "Hatutakuwa na muda wa kukisoma chote. Je, kuna sehemu fulani ungependa mimi nisome?"

"Ndiyo," Nyameye alisema. Alifungua kurasa mpaka akapata hadithi yake anayoipenda. "Je, unaweza kusoma hii, tafadhal? Inaitwa Ndoto ya Lehi."

"Je, hii hadithi ni kuhusu nini? Bw. Otoo aliuliza.

"Kuhusu nabii ambaye aliona ono. Aliona mti mzuri ulio na tunda tamu." Nyameye alionyesha picha ya mti. "Alitaka familia yake pia wale tunda lile pamoja naye. Je, utasoma?" Nyameye akampa mwalimu wake kitabu hicho.

"Bila shaka," Bw. Otoo alisema. Kisha alianza kusoma kwa sauti. Alisoma kuhusu njia nyembamba inayoelekeza kwenye mti. Alisoma kuhusu fimbo ya chuma. Na alisoma kuhusu kushika amri.

Selorm rafiki ya Nyameye alinyanya mkono wake. "Ulikuwa mti wa aina gani?" Alimuuliza Nyameye.

"Sijui," Nyameye alisema. "Lakini tunda likuwa zuri sana. Lazima likuwa hata bora kuliko mti wa maembe!" Kisha Nyameye aliacha kufikiria.

"Kanisani, nilijifunza kwamba tunda huwakilisha upendo wa Mungu. Ndiyo maana lilikuwa tamu sana na maalumu!"

Wakati darasa lilipomalizika, Nyameye alikaa nje kumsubiri mama yake. Alitoa kitabu chake cha Kitabu cha Mormoni ili kusoma zaidi.

"Hiyo ilikuwa ni hadithi nzuri," Selorm alisema. Aliketi karibu na Nyameye. "Je, naweza kusoma nyingine pamoja nawe?"

"Ndiyo!" Nyameye alifungua hadithi nyingine. Walisoma kuhusu Abinadi na Mfalme Nuhu.

Wengi wa wanadarasa wao walikuja kusikiliza. Wakati walipokuwa na maswali, Nyameye aliwajibu. Hata aliwaauliza wao maswali ili kuwahoji kuhusu hadithi walizosoma!

Punde Nyameye alimwona mama yake akitembea kuwaeleke. "Asante kwa kusoma pamoja nami," aliwaambia watoto wengine. Alifunga kitabu na kutabasamu. Alifurahia kwamba marafiki zake walipenda hadithi zake kama vile yeye alivyoipenda. ●



**Ni hadithi gani ya maandiko unayoipenda?**